



MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA (DUWASA)

UTARATIBU WA KUFUATWA ILI KUUNGANISHWA KATIKA MFUMO WA MAJISAFI

1. Hatua za kufuata:

- ❖ Mteja anatakiwa kufika ofisi ya maunganisho ya majisafi na kueleza nia yake ya kuunga maji.
- ❖ Karani wa Huduma kwa Wateja atachukua takwimu muhimu za mteja ikiwa ni pamoja na jina kamili la mteja, nambari ya ploti na bloku.
- ❖ Msimamizi wa maunganisho mapya ya maji kwa wateja atampangia fundi ili afike eneo la mteja kwa ajili ya kufahamu eneo na kutambua uwezekaniko wa kuunga maji pamoja na eneo la karibu la kuunga huduma ya maji kwa umbali usiozidi mita 50.
- ❖ Kwa umbali usiozidi mita 50, fundi bomba wa DUWASA atamtaka mteja mtarajiwa kuwasilisha picha mbili za wakati huo za ukubwa wa pasipoti, mchoro wa ujenzi na barua kutoka kwa jirani inayoruhusu kuunga maji.



- ❖ Iwapo umbali wa eneo la mteja na eneo lilipo bomba ni zaidi ya mita 50, fundi atawasilisha suala hilo kwa Msimamizi wa Maunganisho Mapya ya Maji kwa Wateja ambaye naye atawasilisha suala hilo kwa Mhandisi wa Mipango na Ujenzi kwa mashauriano na baadaye Mhandisi wa Mipango na Ujenzi atashauriana na Meneja Ufundi kwa maamuzi.
- ❖ Baada ya kuwa suala hilo limejadiliwa na kufikiwa maamuzi, fundi atashauri eneo la karibu la kuunga maji na mteja mtarajiwa atalazimika kuomba kuunga huduma ya maji kutoka kwa jirani yake.
- ❖ Fundi wa DUWASA ataandaa orodha ya vifaa vinavyohitajika katika maunganisho ya maji na kuwasilisha kwa msimamizi wa maunganisho ya huduma ya maji kwa wateja ambaye ataviingiza katika fomu maalum.
- ❖ Mteja mtarajiwa atatakiwa kununua vifaa vilivyoinishwa na kwa ubora unaotakiwa na fundi atavikagua vifaa hivyo ili kujiridhisha juu ya ubora wake.
- ❖ Mteja mtarajiwa atafanya malipo DUWASA na kupatiwa stakabadhi kwa gharama ya mita ya maji, uchimbaji na ufukiaji wa mtaro na 20% ya thamani ya gharama ya vifaa na uchimbaji na ufukiaji wa mtaro. Mamlaka haitahusika na mapatano au malipo yoyote yatakayofanywa nje ya utaratibu uliowekwa na Mamlaka.





- ❖ Baada ya kuwa mteja kanunua vifaa na kulipa DUWASA gharama ya 20% ya vifaa na mtaro, Mkandarasi wa DUWASA atachimba mtaro kwa kina kisichopungua sentimita 90 na fundi wa DUWASA atalaza bomba na kufunga viungio na baadaye Mkandarasi atafukia mtaro.
- ❖ Fundi wa DUWASA atatakiwa kuandaa mchoro wa namna bomba litakavyolazwa kwa mteja.
- ❖ Msimamizi wa maunganisho ya huduma ya maji kwa wateja ataandaa taarifa zote za mteja na kuwekwa katika jalada moja na kuombea mita ya maji itakayofungwa kwa mteja. Maombi hayo yatakaguliwa na Meneja Ufundi na kuidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji. Mita itatolewa na Mkuu wa Menejimenti ya Manunuzi na Ugavi baada ya taratibu zote kufuatwa.
- ❖ Endapo mteja atafanya malipo atastahili kupata huduma hiyo ndani ya siku tatu za kazi kuanzia tarehe atakayokuwa amefanya malipo.
- ❖ Iwapo kutakuwa na sababu zisizozuilika zitakazofanya mteja asipatiwe huduma katika muda uliopangwa, Mamlaka itampa mteja taarifa rasmi.
- ❖ Endapo mteja hatakuwa ameridhika na huduma atakayopewa ana haki ya kuwasilisha maoni/malalamiko yake kwa Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA kwa anuani ifuatayo:
- ❖ Fundi atatakiwa kufunga mita kwa urefu usiozidi sentimita 40 ikiwa ni pamoja na kumpatia kadi ya kujaza takwimu za usomaji mita kwa mteja.
- ❖ Mteja atatakiwa kusaini nakala mbili za mkataba wa kufungiwa mita ambapo nakala moja itabaki kwa mteja na ya pili itawasilishwa DUWASA.

2. Gharama zitakazohusika:-

- ❖ Gharama za mabomba na viungio vinavyohitajika kuanzia bomba kuu hadi kufika katika eneo la kiwanja cha mteja.
- ❖ Gharama za kuchimba na kufukia mtaro wa bomba.
- ❖ Gharama za usimamizi (Asilimia 20% ya gharama ya vifaa na uchimbaji wa mtaro).
- ❖ Mteja atatakiwa kujenga chemba ya kuhifadhia mita ya maji ili iwe salama.
- ❖ Msimamizi wa maunganisho ya huduma ya maji kwa wateja atatakiwa kuwasilisha jalada la mteja mpya kwa Afisa Kanda kwa kumbukumbu na utambuzi wa mteja husika katika Kanda.

Mkurugenzi Mtendaji,

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma,
Barabara ya Chimwaga, S.L.P. 431, Simu: +255-26-2324245/2321179
Faksi: +255-26-2320060 Toll Free Calls: 0767000207 / 0767000208
E-mail: info@duwasa.go.tz, cs@duwasa.go.tz, md@duwasa.go.tz

Tovuti: www.duwasa.go.tz



MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA (DUWASA)

UTARATIBU WA KUFUATWA ILI KUUNGANISHWA KATIKA MFUMO WA MAJITAKA

1. Hatua za kufuata:

- ❖ Mteja atajaza fomu ya maombi ya kuunganishiwa katika mfumo wa majitaka. Fomu zinapatikana kwenye ofisi ya majitaka.
- ❖ Mteja atatakiwa kueleza eneo ambalo anahitaji kuunganishiwa huduma ya majitaka.
- ❖ Wataalam wa Mamlaka watafanya ukaguzi (survey) kwenye Eneo (nyumba) ya mteja ili kuangalia uwezekano wa kuunganishiwa majitaka na iwapo uunganishaji huo wa majitaka utahusisha kupitisha mabomba kwenye eneo la mteja mwingine, basi muombaji atapatiwa fomu maalum ambayo itatakiwa kujazwa na mwenye eneo kwa kushuhudiwa na Mwenyekiti wa Mtaa husika ikiwa ni uthibitisho kuwa mwenye eneo ameruhusu upitishaji wa bomba katika eneo lake.
- ❖ Pale itakapohitajika, DUWASA itawasiliana na taasisi kama vile TTCL, TANESCO, Manispaa na TANROADS ili kuepusha usumbufu wakati wa utekelezaji wa kazi ya maunganisho na baada ya maunganisho.
- ❖ DUWASA itaandaa usanifu na makadirio ya gharama ya kazi ya maunganisho na kumpatia mteja ikiwa ni pamoja na taratibu za usimamizi wa kazi.
- ❖ Kwa mteja mwenye akaunti ya majisafi atatakiwa kujaza fomu ya maombi ya maunganisho ya majitaka pamoja na kulipa ada ya maunganisho ya majitaka.
- ❖ Kwa mteja ambaye hana akaunti ya majisafi atatakiwa kuingia makubaliano maalum na DUWASA kabla ya kazi ya kuungiwa majitaka kufanyika.

- ❖ Mteja anaweza kupata taarifa za ukaguzi au gharama za kuunganishiwa katika mfumo baada ya siku nne kuanzia tarehe aliyojaza fomu ya maombi. Taarifa, gharama au maelekezo yoyote kuhusu huduma mteja aliyoomba yatapatikana dirisha aliloombea huduma.
- ❖ Mteja atatakiwa kuchimba mtaro katika ubora unaotakiwa na kununua vifaa vya maunganisho ikiwa ni pamoja na mabomba na viungio vyenye ubora ulioelekezwa na Mamlaka.
- ❖ Gharama zote zinazohusika zitalipwa katika Mamlaka na mteja atapewa risiti inayolingana na malipo atakayoyafanya. Mamlaka haitahusika na mapatano au malipo yoyote yatakayofanywa nje ya utaratibu.

2. Gharama zitakazohusika:-

- ❖ Gharama za kuunganishwa kwenye mtandao wa majitaka (connection fees).
- ❖ Gharama za Vifaa zinazojumuisha bomba za majitaka na viungio vinavyohitajika kuunga bomba la nyumbani kwenye mtandao wa majitaka.
- ❖ Gharama za kuchimba na kufukia mtaro.
- ❖ Gharama za usimamizi (supervision charge).





- ❖ Endapo mteja atafanya malipo atastahili kupata huduma hiyo ndani ya siku nne kuanzia tarehe atakayokuwa amefanya malipo.

3. Mambo muhimu ya kuzingatia kwa wateja wenye maunganisho ya majitaka na wananchi wote kwa ujumla:

- ❖ Usiweke taka ngumu ya aina yoyote katika sehemu za kunawia mikono, bafu au karo la kuoshea vyombo.
- ❖ Hakikisha kuwa sehemu zote zinazopitisha majitaka zina machujio (screen) ili kuzuia taka ngumu zisiingie kwenye chemba au mfereji wa majitaka.
- ❖ Hakikisha kuwa chemba zako za majitaka zina mifuniko ili kuzuia kuingia kwa vitu vinavyoweza kusababisha kuziba kwa mfereji hiyo.
- ❖ Kama maji ya mvua yanaingia katika mfumo wa mfereji wako wa majitaka, hakikisha kuwa umetengeneza chemba ndogo ya kutuliza taka ngumu na uweke chekeche (chujio) katika tundu la kupeleka maji katika mfereji wa majitaka.
- ❖ Ni marufuku kumwaga mafuta ya aina yoyote kwenye mfereji wa majitaka.
- ❖ Hakikisha kuwa mabomba yako ni salama wakati wote na toa taarifa mara tu unapoona dalili za kuvuja kwa bomba.
- ❖ Ni marufuku na ni hatari kufanya matengenezo yoyote kuhusiana na mfereji wa majitaka bila kibali au maelekezo ya Mamlaka.
- ❖ Endapo mteja hatakuwa ameridhika na huduma atakayopewa ana haki ya kuwasilisha maoni/malalamiko yake kwa Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA kwa anuani ifuatayo



Mkurugenzi Mtendaji,

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma,
Barabara ya Chimwaga, S.L.P. 431, Simu: +255-26-2324245/2321179
Faksi: +255-26-2320060 Toll Free Calls: 0767000207 / 0767000208
E-mail: info@[duwasa.go.tz](mailto:info@duwasa.go.tz), cs@[duwasa.go.tz](mailto:cs@duwasa.go.tz), md@[duwasa.go.tz](mailto:md@duwasa.go.tz)

Tovuti: www.duwasa.go.tz